Sekta ya Utalii inavyojivunia ongezeko la Wanyamapori >UK 5

Kisima Cha Maarifa

# FIKRA PEVU

fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

Tovuti: www.fikrapevu.co.tz | ISSN 3456-18 Toleo Na 38 Fikra Pevu Jumatano Machi 5, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100





# Dk.Biteko 'atema' madini

>>Asema Sera na Sheria zinazowekwa zinahimiza matumizi ya Nishati Safi


>>Ataka utumike kujadili na kuweka mipango itakayowezesha matumizi ya Nishati Safi

>>Afungua Mkutano wa Awali EAPCE'25

>UK 2

## CCM yataka Chadema ipuuzwe porojo zake

>UK 2



## Kwaheri mtunzi wa jina la Tanzania

>UK 3

## Watu 20 wakamatwa kwa kula hadharani mchana wa Ramadhani

>UK3




## Waziri Mavunde aifungulia mlango sekta binafsi utafiti wa madini

>>Awasilisha mpango wa Mining Vision 2030

>UK 2

MICHEZO **Mwewe azua kizaazaa kambi ya Yanga**

# Dk.Biteko ahimiza matumizi ya Nishati Safi

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko amesema licha Bara la Afrika kuwa na mchango mdogo katika uchafuzi wa hali ya hewa, nchi za Afrika bado zimekuwa mstari wa mbele katika kuendesha ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuijumuisha katika mifumo yao ya kisheria na udhibiti ikiwemo ya kuhakikisha kuwa nchi zinahama kutoka kwenye matumizi ya nishati chafu na kutumia nishati safi ili kuiepusha dunia na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Dkt. Biteko ameyasema jana wakati akifungua Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) litakaloanza rasmi leo ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG).

Alisema,mkutano wa EAPCE' 25 ni jukwaa muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wadau wengine kujadili mipango na mikakati kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi hasa ikizingatiwa kwa sasa dunia inapambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na shughuli za binadamu huku tafiti za kisayansi zikionesha kuwa viwango vya utoaji wa hewa ya ukaa vimeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Viwanda.

" Nataka nichukue nafasi hii kuwaomba wote muutumie mkutano huu kujadili masuala ambayo yatatufanya sisi wana Afrika Mashariki, tuweze kuhama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyokuwa safi kwenda kwenye matumizi ya nishati iliyosafi, lazima mtambue kwamba mkutano huu wa awali haujatokea kwa bahati mbaya, kama jamii tunayo kazi ya kufanya ya kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda matumizi ya nishati safi." alisisitiza Dkt.Biteko

Ameeleza kuwa, sheria nyingi zinazopitishwa kwa sasa barani Afrika zinahimiza uchumi wa kijani, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuwa na maendeleo endelevu ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa upande wake imeandaa Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni uthibitisho wa dhamira ya kanda hiyo katika kushughulikia tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuhimiza matumizi ya nishati safi.

Alitaja baadhi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi kuwa ni pamoja na ukame mkali, mafuriko, kupotea kwa viumbe hai, kupungua kwa vyanzo vya maji safi, kuyeyuka kwa barafu, na ongezeko la magonjwa yanayohusiana na tabianchi kama vile saratani ya ngozi.

Dkt.Biteko ameeleza kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi linatiliwa mkazo pia katika ngazi ya dunia na hii imepelekea kuwepo kwa mikataba mbalimbali ya kimataifa ukiwemo wa Kyoto, Montreal na Paris ambapo nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinaandaa na kutekeleza mikakati inayohusiana na tabianchi ikiwemo kujikita katika matumizi ya nishati safi zisizochafua mazingira ikiwemo Gesi Asilia.

Kuhusu upatikanaji umeme amesema Afrika ndiyo Bara linalokabiliwa na upungufu mkubwa wa nishati duniani, ambapo asilimia 75 ya watu wanaokosa nishati duniani wanapatikana barani humo lakini juhudi zinafanyika ili kuwezesha upatikanaji wa nishati na hili lilithibitishwa kupitia Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliofanyika Tanzania Januari mwaka huu ambao uliweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030 ambayo ni hatua muhimu kuelekea mabadiliko ya kinishati.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia amesema mabadiliko yanahitajika ili kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi kwani idadi kubwa ya watu barani Afrika bado wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia akitolea mfano nchini Tanzania.

Takriban asilimia 81 ya kaya zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vyao vikuu vya nishati ya kupikia, hali inayosababisha upotevu wa misitu wa takriban hekta 469,420 kila mwaka akitanabaisha kuwa mwelekeo huo wa kutisha unahitaji hatua za haraka na za pamoja ili kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia barani kote.

Alisema,katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni kinara wa ajenda nishati safi ya kupikia kitaifa na kimataifa kwa ujumla amechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034) ambao unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Aidha alisema, matumizi ya gesi asilia kama nishati ya kuendeshea vyombo vya usafiri pia ni muhimu katika kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi akieleza kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuboresha mazingira kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika ujenzi wa Vituo vya Gesi Asilia Iliyoshindiliwa (CNG) na kuboresha sera na mifumo ya udhibiti.

Naibu Waziri Nishati, Judith Kapinga kwa upande wake alisema mkutano huo wa awali unaweka msingi wa Kongamano la 11 la Mafuta kwa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki litakaloanza leo.

"Siku ya leo kutakuwa na mada mbalimbali zitakazozungumzwa, ambazo zitakuwa na majadiliano yatakayoweka msingi kwa ajili ya mkutano mkuu utakaoanza kesho na kufanyika kwa siku tatu, mkutano huu ni muhimu katika kuwaweka wadau pamoja na kujadiliana masuala ya msingi ambayo yatazisaidia Nchi za jumuia ya Afrika Mashariki katika Sekta ya Mafuta na Gesi." alisema Kapinga

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema kuwa mkutano huo wa Mafuta na Gesi unaenda sambamba na Maonesho ya bidhaa za mafuta na gesi pamoja na kazi mbalimbali zinazofanyika katika sekta miongoni mwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alieleza kuwa, Mkutano umelenga kuangalia namna bora ya kuhama kutoka kwenye nishati zinazochafua mazingira kwenda kwenye nishati safi zisizochafua mazingira ikiwa ni kampeni ya dunia ambayo imetokana na malengo ya dunia ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2050 hadi 2060 dunia iwe imeweza kuhamia kwenye nishati safi kwa kiasi kikubwa.

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa, katika mkutano huo nchi zitapata nafasi ya kuelezea maendeleo waliyofanya katika eneo la mafuta na gesi ambapo Makatibu Wakuu na Mawaziri watazungumza kuhusu mafanikio, mipango na kazi zilizofanyika tangu kufanyika kwa mkutano uliopita wa EAPCE.

Alisema,katika mkutano wa EAPCE'25 wataalam, watafiti na wabunifu mbalimbali watazungumzia ugunduzi wa mafuta na gesi, sehemu ambazo vitalu vinanadiwa na kukaribisha uwekezaji kwa nchi za EAC.

# Waziri Mavunde awasilisha mpango wa Mining Vision 2030

Na Mwandishi Wetu,

WAZIRI wa Madini Anthony Mavunde amezikaribisha nchini Tanzania Kampuni za Utafiti wa madini kushirikiana na serikali katika kutimiza malengo ya Mining VISION2030 ambayo imejikita katika kufanya utafiti wa kina wa madini kufikia eneo la ukubwa wa asilimia 50 kufikia mwaka 2030.

Mavunde ameyasema hayo jana jijini Toronto,Canada wakati akihutubia kikao cha Mawaziri wa Madini kutoka nchi mbalimbali duniani,Kampuni za Utafiti na Uendelezaji Migodi na Asasi za kiraia.

"Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia S. Hassan imeweka mazingira wezeshi ya kiuwekezaji,hivyo ni fursa kubwa ya Kampuni za Utafiti kuja kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika mkakati wake wa kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa kina wa madini.

"Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Madini,inatekeleza mpango wa utafiti wa madini wa kina kutoka eneo la utafiti wa kina la asilimia 16 kufikia eneo la asilimia 50 kufikia mwaka 2030,".

"Kwa kuwa Tanzania ni kisiwa cha amani,uongozi imara na mazingira mazuri ya kiuwekezaji nichukue fursa hii kuwakaribisha wadau kuungana na serikali katika mpango wake huu wa utafiti wa kina wa madini nchini kwa kuwa serikali peke yake haiwezi kufanya kwa eneo lote hivyo sekta binafsi ni muhimu katika kufikia azma"alisema Mavunde

Awali akiwa katika mabanda ya maonesho ya vifaa vya Madini,akiongozana na Balozi wa Tanzania nchini Canada Joseph Sokoine na wataalamu wa Wizara ya Madini,Waziri Mavunde amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Dkt. Venance Mwasse kuangalia namna ya upatikanaji wa vifaa vya utafiti wa awali wa madini ili wakati wachimbaji wadogo wakipata huduma ya uchorongaji kuwepo pia vifaa vya awali vya kusaidia kuonesha maeneo yanayopaswa kuchorongwa.



# CCM yaipopoa Chadema

Na Mwandishi Wetu

KATIBU wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayehusika na Itikadi, Uenezi na Mafunzo, CPA Amos Makalla, amewataka Watanzania kupuuza madai ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwamba uchaguzi Mkuu hautafanyika bila mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi.

Akizungumza jana katika kikao cha viongozi wa CCM wa mashina, kata, matawi na mabalozi wa Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Makalla alisema,CHADEMA inakosea kuwaambia wafuasi wao wasijiandikishe kwa madai kuwa hakutakuwa na uchaguzi.

Alisisitiza kuwa uchaguzi Mkuu utafanyika kwa mujibu wa sheria na katiba, na kwamba madai ya CHADEMA kwamba "No Reform, No Election" ni propaganda zisizo na msingi.

Kauli yake inakuja huku mijadala ikiendelea kuhusu mustakabali wa uchaguzi na msimamo wa vyama vya siasa juu ya mazingira ya kisiasa nchini Tanzania.



# Watu 20 wakamatwa kwa kula hadharani mchana wa Ramadhani

Na Mwandishi Wetu

POLISI wa Kiislamu katika jimbo la Kano, kaskazini mwa Nigeria wamewakamata Waislamu 20 waliokutwa wakila mchana hadharani wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambapo pia Watu watano wamekamatwa kwa kuuza chakula huku Naibu kamanda wa Polisi Mujahid Aminudeen akisisitiza kuwa msako huo utaendelea mwezi mzima.

Aminudeen amesema hatua hiyo inalenga kudumisha heshima ya Ramadhan kwani Waislamu wanapaswa kufunga kuanzia alfajiri hadi jua linapozama pia ameeleza kuwa wale waliokamatwa tayari wamefikishwa katika Mahakama ya Sharia kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mbali na hilo Polisi wa kiisalmu wa Hisbah pia wamewakamata Watu waliovaa mavazi yanayokiuka maadili ya Kiislamu wakiwemo waliokuwa na nywele zisizoruhusiwa na Madereva wa Bajaji waliowachanganya Abiria wa jinsia tofauti.

Mfumo wa Sharia umeendelea kutumika katika baadhi ya majimbo ya kaskazini mwa Nigeria kwa Waislamu tangu kuanzishwa kwake zaidi ya miaka 20 iliyopita.

# Buriani mtunzi wa jina la Tanzania

Na Mwandishi Wetu

ATAKUMBUKWA, Mohammed Iqbal, aliyekuwa msomi na mchambuzi wa masuala ya kisiasa, alikuwa miongoni mwa Watanzaia walioshiriki katika mijadala muhimu kuhusu muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Katika harakati hizo, alitoa pendekezo la jina "Tanzania," ambalo lilitokana na mchanganyiko wa majina ya Tanganyika na Zanzibar, na hatimaye likakubaliwa rasmi na viongozi wa wakati huo, akiwemo Mwalimu Julius Nyerere.

Katika mahojiano na waandishi wa habari miaka kadhaa nyumba Mohammed aliwahi kutoa ufafanuzi kuhusiana na jinsi alivyobuni jina hilo loa Tanzania.

Alisema, kwa muongozo wa Mungu alichukua herufi tatu za kwanza za Tanganyika (TAN) na herifi tatu za Zanzibar (ZAN) na kisha akaongeza (I) kutoka kwa jina lake Iqbal na Imani yake katika Uislamu. Hatimaye akakumbuka uhusiano wake na madhehebu ya Ahmadiyya na akaongeza (A) ili kuheshimu madhehebu hayo, na hivyo TANZANIA ikatokea.

Mohammed Iqbal alizaliwa katika kipindi cha ukoloni Agosti 8, 1944 na alihusika kwa kiasi kikubwa katika mijadala ya utaifa na harakati za ukombozi wa Tanganyika.Alikuwa mtu mwenye uelewa wa kina kuhusu historia, utambulisho wa kitaifa, na umuhimu wa mshikamano wa bara na visiwa.

Mnamo mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuunda taifa jipya. Kulikuwa na mjadala wa jina gani lingeweza kubeba dhana ya umoja wa nchi hizo mbili, na hapo ndipo Mohammed Iqbal alipoleta wazo la "Tanzania"—jina lililopokelewa kwa furaha na hatimaye kuwa rasmi.

Katika maisha yake, Iqbal aliendelea kuwa mchangiaji mkubwa katika mijadala ya maendeleo ya kitaifa na umuhimu wa utambulisho wa Tanzania. Kupitia mchango wake, jina "Tanzania" limebaki kuwa alama ya mshikamano wa Watanzania na kiashiria cha historia ya taifa.

Kwa kifo cha Mohammed Iqbal, taifa limepoteza mtu muhimu aliyetoa mchango mkubwa katika historia yake. Serikali, viongozi wa kisiasa, wasomi, na wananchi kwa ujumla wanaendelea kuomboleza kifo chake huku wakikumbuka mchango wake usiosahaulika.

Urithi wa Iqbal utaendelea kuishi kupitia jina "Tanzania," ambalo linawakilisha umoja, mshikamano, na utaifa wa Watanzania wote.Iqbal amefariki akiwa na miaka 80, na chanzo cha kifo chake kimetokana na kuugua kwa takribani miaka 10, na alikuwa chini ya uangalizi wa karibu nyumbani kwake.

# Mzee wa miaka 74 jela kwa kukuua bila kukusudia

Na Mwandishi Wetu

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa imemhukumu kifungo cha miaka minne jela Mzee Chezali Kambole (74) Mkazi wa semtema kwa kosa la kumchoma na kitu chenye ncha kali Filbert Bai (32) anayedaiwa kuwa mdeni wake mkazi wa mtaa huo wa semtema uliopo Manispaa na Mkoa wa Iringa.

Hukumu hii ya kesi ya kuua bila kukusudia imesomwa na Jaji Angaza Mwipopo wa Mahakama kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa, upande wa jamhuri ukisimamiwa na wakili Habati Ishengoma pamoja na Majid Matitu huku upande wa mshtakiwa ukiwakilishwa wakili Jerry Mungo pomoja na Asifiwe Mwanjero.

Imeelezwa mahakamani hapo mshtakiwa ambaye alikuwa akijishughulisha na kazi ya kuuza mipini ya jembe alikuwa akimdai Marehemu fedha kiasi cha shilingi Elfu mbili, siku ya tukio wakiwa kilabuni wanakunywa pombe alikumbushia deni lake na Marehemu anadaiwa kukataa kulipa huku akijibu 'Silipi'.

Baada ya majibizano ya muda Mzee Kambole akaanza kumpiga Marehemu sehemu mbalimbali za mwili wake kisha akachomoa kisu na kumchoma sehemu ya kushoto ya kifua hali iliyopelekea kuvuja damu nyingi na kupelekea umauti wake.

Hata hivyo Mshitakiwa alipopewa nafasi yakujitetea alikiri kutenda kosa hilo huku akiomba mahakama impunguzie adhabu kwani ni kosa lake la kwanza na alikuwa katika hasira iliyochanganyana na ulevi huku akigusia umri wake wa uzee wa miaka 74 na ni tegemeo kwa Familia yake.

Hata hivyo upande wa Jamhuri ukiongozwa na wakili Habati Ishengoma uliendelea kupigilia msumari Mshtakiwa apewe adhabu kali ili iwe fundisho kutokana na historia mbaya iliyopo katika jamii hasa kwa baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi.

# Kuuzwa mali za marehemu kulipia deni lake

NA BASHIR YAKUB -WAKILI

MAREHEMU atakapokuwa ameacha shauri mahakamani ambalo alikuwa anashtakiwa nalo kabla ya kufa kwake basi hukumu itakapotoka itatakiwa kutekelezwa. Hapa tunaongelea hukumu itokanayo na mashauri ya madai.

Sambamba na hilo makala yataangalia pia mambo kadhaa yanayohusu kifo cha mtu ambaye alikuwa akishitakiwa/akilalamikiwa mahakamani kabla ya kifo chake. Amri ya xxii kanuni ya 1 – 12 ya sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai ndiyo itakayotuongoza.

1.JE MSHITAKIWA AKIFA NA KESI ITAKUFA.

Kanuni za jumla (general rule) ni kwamba shauri hutakiwa kufunguliwa na mtu aliye hai dhidi/akimshitaki mtu aliyehai. Hii ni kanuni ya jumla yenye kumaanisha kuwa mtu aliyekufa hawezi kushtaki wala kushtakiwa. Hata hivyo kwenye kanuni za sheria pale penye kanuni ya jumla( general rule) huwa kuna vinginevyo( exception). Hii ina maana yapo mazingira ambapo mshitakiwa atakufa lakini kesi yake haitakufa itaendelea.

2. KESI KUENDELEA HATA BAADA YA KIFO CHA MSHITAKIWA/ MLALAMIKIWA.

Ikiwa marehemu alikuwa ameshtakiwa/amelalamikiwa katika kesi ambazo zinahusu mali kama nyumba, gari, kiwanja na mali nyinginezo na akafa kabla ya kesi hiyo kuisha basi kesi hiyo itaendelea. Pia ikiwa alishitakiwa katika mashtaka yanayohusu masuala ya mikataba pia kesi hiyo nayo itaendelea.

3.KUTOENDELEA KESI BAADA YA KIFO CHA MSHITAKIWA.

Ikiwa mashitaka aliyoshitakiwa nayo marehemu yalikuwa ni mashtaka binafsi basi kesi hiyo haitaendelea. Mashtaka binafsi (personal) ni kama mashtaka ya kudai fidia baada ya kudhalilishwa, kupigwa, kutukanwa n.k., Mashtaka ya namna hii ni mashtaka yenye viashiria vya ubinafsi ( individuality) na hivyo hufa pale tu mshitakiwa anapokufa.

4.NDUGU WA MSHITAKIWA KULAZIMIKA KURITHI MASHTAKA.

Ikiwa mshitakiwa amefariki lakini ikawa kesi yake bado ina hadhi ya kuendelea kutokana na mashitaka yaliyokuwa yakimkabili basi ndugu wa marehemu watalazimika kusimama kama washitakiwa na kuendeleza ile kesi.

Amri ya xxii kanuni ya 4 ( 1 ) ya sheria ya mwenendo wa madai inasema kuwa mshitakiwa anapokuwa amefariki na shauri likatakiwa kuendelea basi mahakama itawezesha mwakilishi wa marehemu mshitakiwa kusimanma badala ya marehemu .

5. KUUZWA MALI ZA MAREHEMU KULIPIA DENI .

Hapa ni deni lile litokanalo na hukumu. Ikiwa kesi imeendelea na hatimaye kutolewa hukumu/ maamuzi basi utaratibu wa kulipa ikiwa kesi inahusu kulipa utafuata. Lakini pia kama kesi inahusu kurudisha mali fulani kama nyumba,kiwanja basi kitatakiwa kurudishwa hata kama marehemu alikirithisha katika wosia.

6. ULAZIMA WA NDUGU KUCHUKUWA KESI YA MAREHEMU MSHITAKIWA.

Ulazima wa ndugu wa marehemu kurithi mashtaka yaliyokuwa yakimkabili ndugu yao unatokana na ukweli kuwa ikiwa watakataa kutokea na kusimama kama washitakiwa wapya na kuendelea kutetea kesi iliyokuwa ikimkabili marehemu basi kesi itaendelea na upande mmoja uliopo yaani upande wa walalamikaji na hukumu itatolewa.

Hukumu itakapotolewa utafuata utekelezaji ambapo mali alizoacha marehemu ndizo zitakazotumika kulipia kile kinachotakiwa.
Kama ni nyumba au kiwanja na kinatakiwa kurudishwa basi kitarudishwa hata kama ndugu wameishagawana. Kwahiyo ni muhimu basi ndugu kujitokeza na kusimama kama washitakiwa wapya katika kesi za namna hiyo. Kujitokeza ni bora kwakuwa kunaweza kubadili matokeo tofauti na kutokujitokeza. Kutokujitokeza maana yake ni nyepesi tu kuwa mmempa ushindi mlalamikaji na kwahiyo muwe tayari kunyanganywa mali za marehemu hata kama mmegawana tayari.

MWANDISHI WA MAKALA HAYA NI MWANASHERIA NA MSHAURI WA SHERIA 0784482959, 0714047241 bashiryakub@ymail.com

**Kanuni za jumla (general rule) ni kwamba shauri hutakiwa kufunguliwa na mtu aliye hai dhidi/akimshitaki mtu aliyehai. Hii ni kanuni ya jumla yenye kumaanisha kuwa mtu aliyekufa hawezi kushtaki wala kushtakiwa. Hata hivyo kwenye kanuni za sheria pale penye kanuni ya jumla( general rule) huwa kuna vinginevyo( exception). Hii ina maana yapo mazingira ambapo mshitakiwa atakufa lakini kesi yake haitakufa itaendelea.**



# Sekta ya Utalii inavyojivunia ongezeko la Wanyamapori



Na Philipo Hassan - Dodoma

WAZIRI wa Maliasili na Utalii,Balozi Dkt. Pindi Chana ameeleza kuwa Wizara imeweza kudhibiti shughuli za ujangili katika maeneo yaliyohifadhiwa na kupelekea ongezeko la idadi ya wanyamapori ikiwemo Tembo, Simba, Chui na Nyati.

Akiwa katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani, yaliyofanyika katika Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma Machi 03 mwaka huu, Balozi Chana anazipongeza taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuendelea kusimamia maeneo yaliyohifadhiwa na kupambana na ujangili.

“Nchi yetu inaongoza kwa idadi kubwa ya wanyamapori, tunayo idadi kubwa ya Simba, Chui, Nyati na niseme kwamba Tanzania ni ya tatu (3) kwa kuwa na idadi kubwa ya Tembo Duniani” anasema Balozi Dkt. Chana.

Naye, Mkurugenzi wa Wanyamapori Tanzania, Dkt. Allex Lobora anaeleza umuhimu wa kuadhimisha siku hiyo ambapo inaikumbusha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili zetu ikiwemo wanyamapori na mimea iliyopo hatarini kutoweka, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia ujangili.

Dkt. Lobora aliongeza “ Siku hii inatoa fursa ya kuonyesha mchango wa wanyamapori katika maisha ya binadamu pamoja na kuhamasisha hatua za kulinda wanyamapori kwa manufaa ya vizazi vijavyo”


Aidha, kaulimbiu ya maadhimisho hayo inasema “Wanyamapori na Uwekezaji Kifedha, Wekeza kwa Watu na Dunia” huku ikihimiza kuwa na mifumo na mikakati endelevu ya kupata na kusimamia matumizi ya rasilimali ili kufikia lengo la uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori.

Maadhimisho hayo yalitanguliwa na maandamano ya amani kutoka Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii Swagaswaga kuelekea Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma ambapo Balozi Dkt. Chana alitembelea mabanda yaliyokuwa yakitoa taarifa kuhusu elimu uhifadhi na utalii.

**Siku hii inatoa fursa ya kuonyesha mchango wa wanyamapori katika maisha ya binadamu pamoja na kuhamasisha hatua za kulinda wanyamapori kwa manufaa ya vizazi vijavyo**



# Unamjua mtunzi wa jina Tanzania?



KIPANDE cha gazeti la The Nationalist la Oktoba 30, 1964.Habari kubwa kwenye gazeti hili na nchi kwa ujumla ni jina jipya la TANZANIA.Ni kwamba baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa April 26, 1964, jina la nchi mpya lilikuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Lakini jina hili lilikuwa refu sana na kuwa kero kwa watumiaji.Serikali kupitia wizara ya habari na utalii chini ya waziri Dkt. Idrisa Abdul Wakili, ikaanzisha mchakato wa kutafuta jina jipya litakalokuwa fupi na rahisi.Ikatoa tangazo kupitia gazeti la Tanganyika Standard, ambalo sasa ni Daily News, kuwataka watanzania wenye kuweza kubuni jina jipya la nchi kufanya hivyo.

Ndipo kijana wa miaka 18 kutoka Morogoro, Mohamed Iqbal Dar, mwanafunzi wa Sekondari ya Aga Khan Morogoro, akaliona tangazo hilo na kushiriki.Akatunga jina la Tanzania na kulituma kwenye anwani iliyotangazwa.

Baada ya muda kupita, akapata barua kutoka serikalini ikimtaja na kumpongeza yeye kama mmoja wa washindi 16 na wakatakiwa kufika ofisi za wizara. Kwa pamoja watu hawa walitakiwa kugawana zawadi ya shilingi 200, wakati huo shilingi moja ilikuwa sawa na dola 8 za Marekani.

Siku ilipofika, watu wawili tu walijitokeza; yeye Mohamed Iqbal Dar na Yusufal Pir Mohamed.

Lakini huyo mwenzake hakuwa na ile barua ya kutajwa kama mshindi na kupongezwa...serikali ikashindwa kumthibitisha hivyo kumtangaza Mohamed Iqbal Dar kama mshindi pekee.

Ndipo Jumatano ya Oktoba 29, 1964 serikali ikatangaza rasmi kwamba jina jipya la nchi ni Tanzania na gazeti la The Nationalist likaichapisha habari hii kubwa, Alhamisi ya Oktoba 30, 1964. Jina la Tanzania likaanza kutumika rasmi Novemba Mosi, 1964.

Alitungaje jina?

TAN - kutoka Tanganyika
ZAN - kutoka Zanzibar
I - kutoka jina lake la Iqbal.
A - kutoka dini yake ya Ahmadiya. Hii pia ikawa rahisi zaidi kwake kwani majina ya nchi nyingi za Afrika yaliishia na A kama Ethiopia, Zambia, Gambia nk.

Ni nani huyu Mohamed Iqbal Dar?
Ni mtoto wa Dkt. Dar, ambaye alikuja Tanzania mwaka 1930 kutoka India. Alifikia Tanga, na ndiko alikozaliwa Mohamed, hakafu akahamia Morogoro.

Mohamed amefarikia huko Birmingham Uingereza

**dipo Jumatano ya Oktoba 29, 1964 serikali ikatangaza rasmi kwamba jina jipya la nchi ni Tanzania na gazeti la The Nationalist likaichapisha habari hii**



# Tuyaenzi maridhiano kwa maslahi mapana ya Zanzibar

Na Sarah Mossi

Takriban wiki kadhaa sasa tumeshuhudia na kusikia matamko mbalimbali kutoka kwa viongozi wa chama kikuu cha upinzani Zanzibar ACT- Wazalendo wakitishia kujitoa kwenye Serikali ya Umoja wa KItaifa iliyoasisiwa na Rais Mstaafu Amaan Abeid Karume na aliyekuwa Mwenyekiti wa CUF wakati huo Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.

Kauli hizi kwa kiasi fulani zimeleta sintofahamu kubwa kwa wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa maana wao ndiio waliopiga kura ya maoni kukubali kuwapo kwa serikali hiyo visiwani hapa.

Ikumbukwe kuwa Serikali ya Umoja wa kitaifa haikuja kwa kubahatisha, Serikali hiyo iliundwa baada ya vyama viwili vilivyoshabihiana kwa karibu sana katika matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa 2000 kukubaliana na hatimaye kutaka maoni ya wapiga kura ambao ni wananchi namna gani wataweza kuendesha serikali na kuondoa ile sintofahamu iliyokuwapo miaka mingi baada nchi kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Haikuwa kazi rahisi kufikia makubaliano hayo kwa maana vyama vyote viwili vilikuwa vikivutia kwake na ilifikia mahali mojawapo ya chama kilitishia kujiondoa kwenye vikao vya kujadili Serikali ya Umoja wa kitaifa huku chama kingine kikitishia kukifufua chama cha Afro Shirazi Party (ASP), mradi tu wagawane mbao.

Lakini hatimaye walifikia makubaliano kwamba amani ya Wazanzibar ni kitu muhimu zaidi kuliko kitu choche na hivyo ukaanzishwa mchakato wa kura ya maoni ambayo hiyo ndio ikatoa mustakabali wa wapi tunaelekea.Serikali ya Umoja wa Kitaifa sio matakwa ya vyama, serikali hii imetokana na maoni ya Wazanzibar wenyewe.

Wazanzibar wenyewe ndio walichagua kuchoka na siasa za uhasama walichagua amani na utulivu ni bora zaidi kuliko chama chochote cha siasa au kuliko kitu chochote. Mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar yaliyoifanya Katiba ya Zanzibar kubadilika yote na kuundwa muundo mwingine wa utawala yaliifanya Zanzibar kutulia kwa kiasi fulani pamoja na kuwapo changamoto kadhaa.

Maridhiano ni jambo muhimu sana katika kuongoza nchi kama zipo changamoto katika kufikia yale makubaliano yaliyozaa serikali hii yanapaswa kushughulikiwa ili kuondoa malalamiko ya mara kwa mara.

Kikosi kazi kilichoundwa kuangalia changamoto mbalimbali katika mwenendo wa kisiasa nchini kinapaswa kuangalia tatizo liko wapi ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili nchi iweze kutulia.Wananchi wa Zanzibar wangependa kuingia kwenye uchaguzi mkuu ujao kwa amani huku wakihakikishiwa usalama wao.

Kama nilivyogusia hapo awli, Serikali hii ilipatikana kutokana na maoni ya kura za wananchi, hivyo wananchi wenyewe bado wanaitaka serikali hii kuendelea mbele. Na kuendelea mbele kwa Serikali hii inapaswa basi kuhakikisha yale makubaliano yafanyiwe kazi kama vile walivyokubaliana.



## KUELEKEA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

# Tanroad Morogoro wakoleza Ujenzi Miundombinu ya barabara



NA VICTOR MAKINDA

WAKATI tunaelekea kwenye maadhimisho ya miaka minne madarakani ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), mkoa wa Morogoro, umefanikiwa kutekeleza miradi miwili mikubwa ya ujenzi wa barabara za lami na kusaini mikataba mipya minne.

TANROADS mkoa wa Morogoro kupitia Meneja wake Mhandisi Razack Kyamba,anasema kwa kipindi cha miaka minne Rais Samia,ameonesha dhamira ya dhati kuhakikisha tatizo la miundombinu ya barabara mkoani humo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mhandisi Kyamba,anasema,ipo miradi ya ujenzi wa barabara ambayo tayari imekamilika huku TANROADS ikiwa imesaini mikataba mingine mikubwa ya ujenzi wa barabara muhimu zinazounganisha wilaya za mkoa wa Morogoro ambapo kukamilika kwake kutachochea kasi ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

" Katika kipindi cha miaka minne ya Rais Samia, TANROADS Morogoro imetekeleza mradi wa barabara ya lami kutoka Rudewa mpaka Kilosa mjini barabara yenye urefu wa Kilometa 24 na madaraja matatu ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 32.9 zimetumika, mradi huo tayari umekamilika" Anasema Mhandisi Kyamba.

Mhandisi Kyamba anautaja mradi mwingine unaotekelezwa na TANROADS mkoa wa Morogoro kuwa ni mradi wa ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa Kilometa 66.9 kutoka Kidatu mpaka Ifakara wilayani Kilombero uliogharimu Shilingi Bilioni 104.

Anasema kuwa mradi huo upo kwenye hatua za mwisho kukamilikaa ambapo kukamilika kwake kutakuwa chachu kubwa ya kukuza uchumi wa wananchi wa wilaya ya Kilombero inayokaliwa na wakazi wengi ambao ni wakulima wazalishaji wakubwa wa zao la mpunga, miwa na mazao mengine ya biashara na chakula.

Anaongeza kuwa mradi wa barabara ya Kidatu Ifakara una umuhimu mkubwa katika kukuza shughuli za utalii kwa kuwa barabara hiyo inapita pembezoni mwa Hifadhi ya Milima ya Udzungwa.

## MIKATABA YA MIRADI YA UJENZI WA BARABARA ILIYOSAINIWA

Mhandisi Kyamba anasema,katika mwaka uliopita wa fedha, TANROADS mkoa wa Morogoro ilisaini mikataba mipya minne ya ujenzi wa barabara za lami.

" Tumekwisha saini mkataba ya ujenzi wa barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mbingu, wilayani Kilombero barabara yenye urefu wa Kilometa 62.5 tayari mkandarasi HEGO amekwisha anza kazi, sambamba na ujenzi wa barabara hiyo kutoka Mbingu kwenda Chita Kilometa 37.5 ambao pia mkataba umekwisha sainiwa. Anasema Mhandisi Kyamba.

Anautaja mkataba mwingine wa ujenzi wa barabara uliokwisha sainiwa ni barabara ya kutoka Bigwa mpaka Kisaki kilometa 78.

"Upo mkataba mwingine wa ujezi wa barabara ya kutoka Ubena Zomozi kwenda Ngerengere Kilometa 10 ambao tayari umesainiwa na mkandarasi anatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni."

Mhandisi Kyamba anasema kuwa sambamba na ujenzi wa barabara hizo za lami TANROADS Morogoro inatarajia kutekeleza mradi wa ujenzi wa madaraja ya korofi ambayo hufurika maji wakati wa masika na kupelekea wananchi kushindwa kuvuka ambayo ni Nguyani na Chakwale wilayani Gairo.

Anasema kuwa Rais Samia amekwisha ridhia ujenzi wa madaraja hayo muhimu na tayari kibali cha ujenzi kimetoka, zabuni za ujenzi huo itatangazwa hivi karibuni na utakapopatikana mkandarasi ujenzi utaanza mara moja.

## UJENZI BARABARA STESHENI YA TRENI RELI YA MWENDOKASI

Injinia Kyamba anasema kuwa TANROADS mkoa wa Morogoro ilipokea maelekezo ya serikali ya kujenga barabra za kuingia kwenye kituo cha Treni ya Mwendokasi (SGR) mkoa wa Morogoro.

Katika kutekeleza agizo hilo wakala huo upo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba kwa kuwa zabuni za ujenzi wa barabara za lami kuingia stesheni hiyo zilikwisha tangazwa.

" Ujenzi wa barabara ya kuingia stesheni ya mwendokasi mkoa wa Morogoro yenye jumla ya Kilometa 13 unatarajiwa kuanza hivi karibuni tukitarajia kuwa ujenzi huo utawarahishia abiria na mizigo kuingia na kutoka stesheni hapo ". Anasema Mhandisi Kyamba.

Mhandishi Kyamba anasema kuwa TANROADS mkoa wa Morogoro unampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake ulitukuka unaojali maslahi ya wananchi na wao TANROADS watazidi kumuunga mkono kwa kufanya kutekeleza wajibu wao kwa weledi, bidii na maarifa.

# Miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Samia, Tanzania imepiga hatua kubwa

Na Mwandishi Wetu

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan anaelekea kutimiza miaka minne madarakani kama mkuu wa nchi, baadhi ya watu wameanza kutoa maoni mbalimbali kuhusu uongozi wake.

Wengi kati ya waliotoa maoni yao ama kupitia vyombo vya habari ama majukwaa mengine rasmi, wamempongeza Rais Samia wakisema uongozi wake umeibadili Tanzania kutoka sehemu moja kwenda mbele zaidi.

Ikumbukwe, Rais Samia aliingia madarakani mwezi Machi 2021 kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Dkt John Magufuli. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikampa Dkt Samia ambaye alikuwa Makamu wa Rais, ikampa nafasi ya kuapishwa kuwa kiongozi mkuu wa taifa hili.

Wakati anaingia madarakani, Rais Samia aliwaahidi Watanzania kwamba ingawa walikuwa wanamlilia Dkt Magufuli, lakini uongozi wake ulikuwa na lengo la kuwafuta machozi Watanzania.Utekelezaji wa kauli yake ulianzia kwenye marekebisho ya sera zinazoongoza vyombo vya habari, ambapo Rais Samia alilegeza baadhi ya masharti yaliyokuwa yanawabana Wanahabari katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kila mwenye akili ambazo hazina mashaka anajua kwamba serikali ilikuwa imeweka baadhi ya masharti magumu katika sera na sheria nzima inayosimamia vyombo vya habari, lakini baadhi ya magazeti yalisimamishwa, lakini pia vyombo vingine vinavyotoa huduma ya habari ikiwemo mitandao ya kijamii vilitikiswa.

Lakini Dkt Samia alijua kwamba mojawapo ya njia nzuri ya kupata maoni kwenye utawala wake ni pamoja na kuruhusu uhuru wa vyombo vya habari kwa kuvipa wigo mpana zaidi wa kufanya kazi zake.Sio hivyo tu, Rais aliamua kuwapa nafasi wanasiasa kufanya mikutano yao na siasa nyingine za kiungwana bila kuzuiwa na mtu, kama siasa hizo zitakuwa hazivunji sheria.

Wote ni mashahidi, na kila mmoja ameona kwamba mikutano ya hadhara ambayo ilikuwa imepigwa marufuku iliruhusiwa tena, lakini kwa mara ya kwanza katika historia ya siasa za upinzani hapa Tanzania, wanachama wa vyama vya upinzani waliruhusiwa kufanya maandamano ili kufikisha ujumbe wao kwa serikali na jumuiya ya kimataifa.

Lakini katika eneo hilo la siasa, Rais Samia amemua kuvunja makundi kwa kuwaunganisha tena watendaji mbalimbali waliwemo wale ambao walikuwa wametupwa nje katika awamu ya tano kwasababu mbalimbali na kuwapa nafasi ili kuleta uwiano.

Mashirika na taasisi mbalimbali za umma waliongezewa uwezo wa kufanya kazi zaidi, lakini baadhi yake zikapewa uhuru wa kuamua baadhi ya mambo yake na kusaidia taasisi hizo kuongeza tija zaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miaka minne ya Rais Dk.Samia Kamishina wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania(TFS) Profesa Dos Santos Silayo anasema katika kipindi cha miaka minne ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan wanajivunia uongozi wake ambao unajali na kuthamini uhifadhi.

Tunatoa shukrani na kumpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka minne na katika jambo ambalo sekta ya misitu tunajivunia katika uongozi wake ni kuwa na kiongozi wa juu anayejali na kuthamini uhifadhi.

Akaongeza: Rais Samia anatoa msukumo wa moja kwa moja yeye binafsi kwenye hilo tunamshukuru sana Rais Dkt. Samia kwani katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake tumefanikiwa kuimarisha uhifadhi wa misitu na misitu yetu imeendelea kushamiri,

Ametuongezea nguvu katika kupata maofisa na askari wa kulinda misitu yetu tumeajiri takriban askari 500 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia. Tumeboresha miundombinu yetu kwa ajili ya kupata ofisi na makazi ya maofisa na askari wetu, anasema Prof. Silayo.Aidha anasema kwa kipindi cha miaka mitatu peke yake wamewekeza Sh. bilioni 31 ambazo zimesaidia kujenga ya ofisi 88 kote nchini ya ofisi lakini wamenunua magari na mitambo ya kutosha.

Takriban Sh.bilioni 18 zimetumika katika kipindi cha miaka mitatu na tumepata magari kwani tunayo magari madogo 113, mitambo 17, boti 10 na pikikipiki 164 katika kipindi cha miaka mitatu.Nayo Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imesema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan migogoro saba imetatuliwa na kubaki mmoja ambao uko hatua za mwisho.

Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA Mabula Misungwi Nyanda anasema mafanikio ya miaka minne Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, Jijini Dar es Salaam.Anasema katika migogoro katika TAWA ilikuwa inanyima usingizi lakini kutokana msukumo wa Rais umewezesha kutatua na kupunguza migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya Hifadhi na wananchi.

Anasema kuwa kwa ushirikiano huo migogoro ya mipaka katika Mapori ya Akiba saba (7) ya Swagaswaga, Mkungunero, Wamimbiki, Igombe, Liparamba, Mpanga Kipengere na Selous kati ya nane (8) yaliyotolewa maelekezo na Kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta imemalizika ambapo jumla ya vigingi 1,681 vimesimikwa kuzunguka mipaka ya hifadhi .

Aidha, anasema kuwa katika utatuzi wa migogoro hiyo eneo lenye ekari 103,544.48 limemegwa kutoka kwenye hifadhi na kuwapatia wananchi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwamba Serikali kupitia TAWA inaendelea kukamilisha zoezi la kulipa fidia kaya 145 zilizo katika Pori la Akiba Mkungunero.

"Tumejipanga na tuna kazi kubwa ya kufanya maeneo hayo ili kuokoa maisha ya watu wasidhurike na wanyama wakali na waharibifu ameongeza.Kamishna Nyanda anasema TAWA imejiwekea mipango mikakati imkatika utatuzi wa migogoro hiyo, ambapo eneo la ekari 103,544.48 limetengwa kutoka kwenye hifadhi, na kuwapatia wananchi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

Katika sekta ya Elimu, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimesema katika miaka minne ya uongozi wa Dkt. Samia kinajivunia mafanikio kadha wa kadha ikiwemo ongezeko la udahili wa wanafunzi ziadi ya 3800, kutoka wanafunzi 13,0199 mwaka 2021 hadi wanafunafu 17, 084.

Katika ongezeko hilo wanafunzi 105 kutoka nje ya mipaka ya Tanzania, 22 kati yao wanasoma Shahada za Awali na 83 Shahada za Juu huku kwa upande wa watanzania, wanaume 10, 255 na wanawake 6, 829 kati yao wanafunzi 16,023 wanasoma Shahada za Awali na 1, 061 Shahada za Juu.

Akizungumza na Waandishi wa habari Ofisini kwake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda amesema, ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi kutoka nje ya mipaka ya Tanzania limetokana na mashirikiano mazuri, kuimarika kwa Diplomasia, kazi kubwa inayofanywa na Dkt. Samia ndani ya miaka yake minne ya uongozi.

Kuelekea miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, Tanzania imepiga hatua kubwa lakini wale waliokuwa wanasema wanawake hawawezi kubeba dhamana ya madaraka makubwa ukiwemo Urais, nao wamekuwa mstari wa mbele kumpongeza Rais Samia kwa mambo makubwa aliyoifanyia Tanzania katika miaka yake hii mitatu.




# Dk.Nchimbi mtu sahihi katika wakati sahihi

Na Mwandishi Wetu

INAWEZA kuonekana kama nimchelewa kuandika kitu kuhusu Dk.Emmanuel Nchimbi kuhusu kuteuliwa kwake mgombea mwenza wa Rais Dk.Samia katika uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Kwakuwa kalamu yangu haijaisha wino wacha niandike najua utanielewa tu.lakini nasema bado nipo ndani ya muda sahihi kufanya hivyo.Kwanza niipongeze CCM kufanya Mkutano Mkuu Maalumu uliomteua Dk.Samia Suluhu Hassan umefanyika kimkakati, lakini pia umefanyika kwa muda muafaka kama surprise, lakini kwa kuzingatia sheria na katiba ya CCM, bila kuathiri kwa namna yoyote ile sheria na katiba ya nchi kuhusiana na masuala ya uteuzi wa wagombea uongozi na uchaguzi wenyewe.

Azimio la kumuidhinisha Dk. Emmanuel Nchimbi kama mgombea mwenza wa uraisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilitolewa hadharani na mkutano mkuu maalumu wa CCM taifa, na kuidhinishwa kwa kauli moja za wajumbe wa mkutano mkuu huo maalumu, kwa uthibitisho wa kura za ndio za wajumbe wote wa mkutano mkuu wa Taifa waliohudhuria mkutano ule.



Aina na namna ya uteuzi wa Dk.Nchimbi ulivyofanyika,kwanza imedhibiti makundi ndani ya chama na kuifanya CCM kua moja, yenye nguvu na imara zaidi.Lakini pia hili limedhihirsha umadhubuti wa CCM na thibitishia ulimwengu kwamba CCM ni jabali la siasa za Tanzania na Africa kwa ujumla.

Umadhubuti na umahiri wa Dk.Samia Suluhu Hassan kiutendaji, utampatia uzoefu na uthubutu wa kutosha Dk.Emmanuel Nchimbi kushika hatamu na dhamana ya uongozi wa kitaifa kwa wakati muafaka.

Kama ilivyo mipango ya maendeleo ya vipindi vifupi, vya kati na vipindi virefu, Chama Cha Mapinduzi CCM, kimetoa uelekeo wa uongozi wa kisiasa waTaifa letu kwa kipindi cha miaka 15 ijayo utakuaje.

Na mpango wa usimamizi wa maendeleo na mustakabali wa uongozi wa Taifa letu ni kwamba, 2025-2030 ni Dk.Samia Suluhu Hassan, na kisha kwa Neema na Baraka za Mungu 2030-2040 ni Dk. Emmanuel Nchimbi.

**"Kwakuwa kalamu yangu haijaisha wino wacha niandike najua utanielewa tu.lakini nasema bado nipo ndani ya muda sahihi kufanya hivyo.Kwanza niipongeze CCM kufanya Mkutano Mkuu Maalumu uliomteua Dk.Samia Suluhu Hassan**

# Ni kwa namna gani Upendeleo wa Kijinsia huwakwamisha Wanawake kushiriki katika Siasa Tanzania?

Na Maryam Nassoro

NILIINGIA katika siasa kwa sababu, niliona masuala mengi ya wanawake hayaingii kwenye sera mipango na bajeti kwa kuwa, nafasi nyingi za maamuzi zimeshikiliwa na wanaume.

"Hiyo ni kwasababu ya kushamiri kwa "Mifumo Dume" katika vyama vya Siasa nchini, nilitamani kuingia kwenye uongozi kufanya jambo la ziada kwa kuhakikisha masuala yanayohusu Wanawake na makundi mengine, yanaingia kwenye sera, mipango na bajeti, binafsi niliamini kila mwanamke ni kiongozi, anahitaji tu uthubutu na kuamua kushika hatamu."

Hizo ni kauli za Lucy John Mtembo mwenye miaka 40 ni miongoni mwa Wanachama hai wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja).

Alianza harakati za siasa Miaka ya 2010, ambapo enzi hizo nafasi za uongozi kama Udiwani, Uwakilishi na Ubunge ulikuwa unashikiliwa na Wanaume wengi huku Wanawake wakionekana kuwa ni wapiga debe tu katika kampeni.

Anasema "Nimejifunza kuwa tunapaswa kuwa na uthubutu na utayari kujifunza mambo mapya na kujiwekea mipango inayotekelezeka ili tuwe viongozi wazuri."Lucy anaeleza kuwa bado Wanawake wapo kidogo katika nafasi za uongozi na vyombo vya maamuzi.

Takwimu zinaonesha Zanzibar, hadi sasa kuna wanawake nane tu, waliowahi kugombania nafasi za uongozi majimboni, ambao walishinda uwakilishi, wanawake 18 walipata uwakilishi kupitia nafasi za viti maalum na hivyo, kufanya idadi ya wanawake katika Baraza la Wawakilishi kuwa 29 kati ya 77 waliyochaguliwa sawa na Asilimia 40.

Fatma Abdul Habib Ferej ni Katibu wa Ngome ya Wanawake wa Chama cha ACT Wazalendo, ambaye aliwahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, amesema bado wanawake wako kidogo katika nafasi za uongozi jambo ambalo linahitaji kuangaliwa.

Anna ameongeza kuwa Serikali inaendelea na jitihada katika kufikia malengo yaliyowekwa kupitia Dira ya 2050 na Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021/2026 ambapo lengo katika nafasi za uongozi ni kufikia 50/50

Ripoti ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Tanzania ya Mwaka 2022, inaonesha Zanzibar ina Wakaazi milioni 1.8 kati ya hao wanaume ni 915,492 na wanawake ni 974,281.hii ina maana kwamba wanawake ni Asilimia 51.6 ya Wakaazi wote wa Zanzibar, lakini wingi huo hauonekani katika nafasi za uongozi.

Chama cha Wandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (TAMWA ZNZ) ni Taasisi isiyo ya kiserikali, inayojishuhulisha na masuala ya utetezi wa haki za mtoto wa kike na kuhamasisha wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA ZNZ, Dk. Mzuri Issa amesema vyama vingi vya siasa nchini, vimetawaliwa na mfumo dume jambo ambalo linawarudisha nyuma wanawake kugombea nafasi za uongozi.

Naibu Msajili wa vyama vya Siasa Tanzania, kwa upande wa Zanzibar Mohamed Ali Ahmed amesema kuongezwa kwa kifungu cha 10 C ndani ya Sheria ya Vyama vya Siasa nchini, kinatoa nafasi kwa wanawake kuongeza ushiriki wao.

**"Hiyo ni kwasababu ya kushamiri kwa "Mifumo Dume" katika vyama vya Siasa nchini, nilitamani kuingia kwenye uongozi kufanya jambo la ziada kwa kuhakikisha masuala yanayohusu Wanawake na makundi mengine, yanaingia kwenye sera, mipango na bajeti, binafsi niliamini kila mwanamke ni kiongozi, anahitaji tu uthubutu na kuamua kushika hatamu."**



# Ushindi wa kishindo kwa Rais Samia utachochewa na mgombea mwenza Dk.Emmanuel Nchimbi



Na Mwandishi Wetu

NI wazi,utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM kwa zaidi ya 95% chini ya serikali sikivu ya CCM inayoongozwa na Rais kipenzi cha waTanzania wote Dk. Samia Suluhu Hassan kutamfanya achaguliwe tena kwa kishindo, kumalizia ngwe yake ya pili muhimu sana ya uongozi wa kitaifa kikatiba.

Kuaminika na kukubalika kwa Dk.Emannuel Nchimbi kwa wananchi na waTanzania wote, kumechochea umoja na kuiimarisha CCM kwa kiasi kikubwa, huku ikiwakatisha tamaa na kuwadhoofisha wapinzani kwa kupoteza matumani kabisa ya kupata kiti hata kimoja kwenye uchaguzi mkuu wa udiwani, ubunge na hata URAIS.

Kuimarika, kuaminika na kukubalika kwa CCM kwa wananchi na waTanzania kwa ujumla, kama ilivyo sasa, ni matokeo ya mabadiliko ya uongozi wa juu wa chama na serikali sikivu ya CCM, na ufanisi wa kiwango cha juu sana katika katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya 2020-2025 kwa ubora na viwango vya kimataifa.

Wakati vyama vingine vya kisiasa viko usingizini na vingine vikibabaika na mjadala wa kuunganisha nguvu ama laa, Chama Cha Mapinduzi CCM tayari kimeshakamilisha maandalizi muhimu ya ndani kuhusu uchaguzi huo wa oct.2025.

Ni suala la muda tu wa kisheria na kikatiba ndio unasubiriwa.Na hii ni ishara ya wazi na maandalizi kabambe ya ushindi wa kishindo mathalani kwenye nafasi ya urais, ambayo tayari mgombea urais Dr.Samia Suluhu Hassan na mgombea mwenza wake Dk.Emmanuel Nchimbi, wanafahamika kwa waTanzania wote, wanakubalika na kuaminika kwa wananchi kuliko mwanasiasa yeyote nchini Tanzania.

Kwa kwa uzoefu wako katika siasa za Tanzania, na kwa kuzingatia hali ya siasa na kukubalika kwa wagombea hao makini wa chama tawala, unadhani CCM inaweza kupata ushindi wa chini ya 90% kweli kwenye uchaguzi wa Oktoba 2025.Mambo haya yataongeza kwa kiwango na uhakika wa ushindi wa kishindo kikuu, kwa wagombea udiwani, ubunge na uraisi wa CCM mwaka huu.

*Kidumu Chama Cha Mapinduzi*
*Mungu Ibariki Tanzania*

**Wakati vyama vingine vya kisiasa viko usingizini na vingine vikibabaika na mjadala wa kuunganisha nguvu ama laa, Chama Cha Mapinduzi CCM tayari kimeshakamilisha maandalizi muhimu ya ndani kuhusu uch**

# Tubaki ama tuhame? Raia wagaza wako njia panda

Ukitazama eneo la Jabalia, ukiwa angani, inatamausha.Taswira ambayo inaonyesha uharibifu mkubwa.Majengo yaliyoporomoka, vifaa vilivyoning'inia na vifusi vilivyogeuka mlima wa taka.

Kutokana na hali hii ya majengo ni vigumu kubaini mandhari halisi ya eneo hilo.

Lakini ukitumia kamera zinazotumia ndege zisizo na rubani utaona mahema ya buluu na meupe ambapo kambi zimeanzishwa katika eneo tambarare.Na katika pita pita zako utaona masoko yaliyochipuka kando ya vifusi, taka zimetapakaa na watoto wakibembea kwa vyuma vya vifusi vya majengo yaliyoporomoka.

Baada ya wiki sita ya makubaliano yakusitisha mapigano kutekelezwa, eneo hili la Jabalia limeanza kuchipuka upya huku shughuli za kawaida zikianza kurejea.Nabil akiwa amesimama karibu na vifusi vya nyumba yake aliyoiacha wakati wa vita. Wengi, kama Nabil, walioirudi makwao wamekuta nyumba zao zimeharibiwa au zimeporomoka.

Katika eneo jirani al-Qasasib, Nabil amerejea kwa nyumba yake ya ghorofa nne ambayo kidogo iko katika hali mtu anaweza kuishi, lakini haina madirisha, milango na upande mwingine haina ukuta.

Akiwa na familia yake wamebuni kuta kwa kuweka mbao na kugongelea ili zisianguke.''Hebu angalia uharibifu huu,'' anasema huku akikagua vifusi vya nyumba yake aliyoienzi.

''Wanataka tuhame bila ya kujenga upya makazi yetu? Tutahama vipi. Kile tunaweza kufanya ni kukarabati upya kwa ajili ya watoto wetu.''Akianza pilka pilka za mapishi, Nabil anawasha moto katika ngazi yake akitumia mbao zilizoharibika wakati wa majengo kuporomoka.

**'Wanataka tuhame bila ya kujenga upya makazi yetu? Tutahama vipi. Kile tunaweza kufanya ni kukarabati upya kwa ajili ya watoto wetu.''Akianza pilka pilka za mapishi, Nabil anawasha moto katika ngazi yake akitumia mbao zilizoharibika wakati wa majengo kuporomoka.**



Katika Chumba kingine, Laila Ahmed Okasha anafanya usafi karo ambayo maji ya mfereji yaligoma miezi kadhaa iliyopita.'' Hakuna maji, stima na pia mabomba yakupitisha maji taka,'' anasema.''Iwapo tunahitaji maji inatulazimu tusafiri maeneo ya mbali ,''Anasema alibwaga kilio aliporejea nakupata nyumba yake kuwa gofu .Analaumu Israel na Hamas kwa kuharibu mahali alipopaita nyumbani.''Wote ni wa kulaumiwa,''anasema .'' Tulikuwa na makazi mazuri na tuliishi maisha yasio na bughudha''.

Baada ya vita kuanza mwezi Oktoba 2023, Israel iliwaarifu Wapalestina wanaoishi katika ukanda wa Gaza- ikiwemo Jabalia- kuhamia maeneo ya Kusini kwa usalama wao.Mamia ya maelfu ya watu waliitia wito huo, lakini baadhi walikaidi amri na kuapa kuhimili vita vilivyokuwa vikichacha.

Laila na mumewe Marwan walikuwa wamesalia hadi mwezi Oktoba mwaka jana, ambapo wanajeshi wa Israel walivamia tena Jabalia, kwa madai Hamas walikuwa wakijikusanya upya katika kambi waliokuwa wamejihifadhi.Baada ya miezi miwili ya kupata uhifadhi katika kambi iliyo karibu ya Shati, Leila na Marwan walirejea Jabalia na kupata hali imegeuka na yakusikitisha.



# Kinachoitesa Man United ni wachezaji na makocha waliotangulia siyo Amorim

**OLE Gunnar Solskjaer amefichua na kusema anajua ni wapi penye shinda kwenye kikosi cha Manchester United kinachofanya hovyo chini ya Ruben Amorim na kudai sio kosa la kocha.**

Man United imekuwa kwenye kiwango duni tangu ilipokuwa chini ya Mreno huyo aliyekuja kuchukua mikoba ya Erik ten Hag huko Old Trafford. Amorim ameshinda mechi tano tu kati ya 16 alizoiongoza timu hiyo kwenye Ligi Kuu England, huku kikosi hicho kikishika nafasi ya 14 kwenye msimamo.

Wachezaji kibao wa Man United wanapambana na hali kufiti kwenye mtindo wa kiuchezaji wa kocha Amorim wa 3-4-2-1. Na Solskjaer, ambaye alikuwa straika wa Man United kabla ya kuwa kocha wa miamba hiyo ya Old Trafford anachoamini ni kwamba tatizo linaanzia kwa wachezaji sio kwa Amorim ni makocha waliomtangulia.

Alipoulizwa kwa nini kuna kufukuzana sana Man United au huo ndio utamaduni wao, Solskjaer alijibu: "Hiyo ni kwa mabosi wa juu wa Man United, lakini ishu pale ni kocha kutumia wachezaji waliosajiliwa na makocha wengine.

"Nakumbuka nyakati nzuri nilipokuwa Man United nje ya zile wiki sita za mwisho. Watu wao ni safi na utamaduni ni watu. Kurudi Man United ni kama kurudi kwa familia tangu.. kama vile nilikuwepo tu muda wote.

"Lakini hapa Besiktas najiona kama familia pia, watu waheshimiana sana. Kuna watu hapa wamekuwa na timu hiyo kwa miaka 10, 20 hadi 30."

Solskjaer, 52, aliinoa Man United karibu miaka mitatu, hakubeba taji hadi hapo alifunguliwa mlango wa kutokea Novemba 2021 kufuatia kichapo cha kushtua kutoka kwa Watford. Na wakati mambo yakienda kombo kwa Solskjaer alipokuwa Man United, mwenyewe anajivunia kwa kile alichokifanya kwenye timu hiyo licha ya changamoto zote.

"Zile wiki sita za mwisho zilikuwa ngumu sana, siwezi kukataa, lakini tulikuwa vinara kwenye kundi letu la Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Solskjaer.

"Ni zile mechi mbili dhidi ya Man City na Watford ndizo zilizotibua, lakini nilipambana timu ilimaliza nafasi ya pili na tatu katika misimu yangu miwili mizima niliyokuwa kwenye timu na Man United haikuwa mbaya sana kwenye Ligi Kuu England.

**Zile wiki sita za mwisho zilikuwa ngumu sana, siwezi kukataa, lakini tulikuwa vinara kwenye kundi letu la Ligi ya Mabingwa Ulaya,**



FIKRAPEVU
MICHEZO
JUMATANO, MACHI 5 2025



# Mwewe azua kizaazaa kambi ya Yanga SC

Na Mwandishi Wetu

ZIKIWA zimesalia siku tatu kabla ya kupigwa mechi ya watani wa jadi kisoka Yanga na Simba kumeibuka sintofahamu ndani ya kambi ya wananchi baada ya ndege jamii ya mwewe kutua kwenye mazoezi ya timu hiyo na kuondoka na bibs.

Taarifa ambazo gazeti hili,limezipata zinaeleza tukio hilo linahusishwa na mambo ya kishirikina kwani bibs iliyochukuliwa ilikuwa imevaliwa na mmoja ya mastaa wa timu hiyo hivyo kufanya mkasa huo kuzua hofu kwa mashabiki wa Yanga kuelekea mchezo huo.

Tukio la mwewe huyo kuondoka na bibs ya mchezaji huyo linaelezwa kuwachanganya mashabiki wa timu hiyo wakiamini ni njama iliyosukwa na mahasimu wao Simba kama njia ya kuwavuruga kisaikolojia.

Kwa nyakati tofauti wa Yanga umegoma kuthibitisha ukweli wa mkasa kuogopa kuwatoa kwenye reli wachezaji na mashabiki wa timu hiyo kwani itakumbukwa wananchi ndiyo wenyeji wa mchezo huo utakaopigwa Jumamosi kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Imekuwa ni kawaida inapokaribia au siku ya mchezo wenyewe uwanjani baina ya timu hizo kuibuka matukio mbalimbali yenye sura za kishirikina jambo ambalo huziweka pagumu kambi za timu hizo kabla ya mechi kupigwa.

Kuelekea mchezo huo joto limekuwa likipanda kila kukicha kwani ni mechi yenye mahitaji makubwa kwa timu zote mbili ambapo Yanga inahitaji kushinda ili kutanua wigo wa pointi dhidi ya mtani wake lakini kwa Simba wanataka kuchonga barabara ya kuwapoka watani zao taji la ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Yanga wapo kileleni mwa msimamo na pointi zao 58 wakati Simba ipo nafasi ya pili na pointi zake 54.



# Simba yaivaa Yanga na hesabu kali

Na Yassir Sudi

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davis amesma anazihitaji kwa udi na uvumba alama tatu kutoka kwa mahasimu wake wa jadi Yanga kuelekea mechi baina ya timu hizo itakayopigwa Jumamosi uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili Fadlu,alisema,anajua mechi hiyo ndiyo itakayotoa sura ya nani atakayekua bingwa msimu huu hivyo kushinda kwake ni jambo la lazima.Alisema,anajua Yanga ni timu bora na iliyoshikana muda mrefu lakini hana wasiwasi na kikosi chake kwani wachezaji wake wanajua umuhimu wa kushinda mchezo huo.

Fadlu, alisema,Jeshi liko tayari kwa vita yoyote iliyo mbele yao kwani wamejipanga kumaliza kwa kushinda mechi zote za mzunguko wa pili ili kutwaa taji hilo kwa kishindo.

"Niaheshimu Yanga kama bingwa mtetezi mwenye kikosi kilichoshikana muda mrefu lakini hiyo kwetu siyo kitu kwetu kwani tunachotazama ni kupata alama tatu ili kujiweka sawa na mbio za ubingwa wa Ligi Kuu,"alisema Fadlu.

